# DUNIA INASAMBARATIKA

Gosbert Damazo



KIITIKIO:




2.Watu wamkwepa Mungu (jamani) hawaendi kumuabudia
Waenda kwa Ibilisi (jamani)kwa hizo zake nyingi anasa
Njoo), njoo roho wa Ibada njoo roho wa Imani mfukuze shetani
(njoo)Twongoze katika kwe(Roho)) tumjue Mungu wetu(Roho)
(Kaa)kaa nasi utuimarishe utukinge na mwovu shetani (kaa nasi) tuepushe na shetani

KIITIKIO:Dunia,Dunia inasambaratika,maadili yanamomonyoka.
Mizigo,mizigo imetuelemea Roho, Roho wa Bwana usituache

3.Ubakaji wa watoto (jamani) ulawiti vimezidi
ndoa za jinsia moja (jamani)mbona zajengewa hoja
(Hivi) mambo gani tunafanya mbona aibu hatuna twamchukiza Mungu
(Njoo )Njoo roho mwenye nuru(Roho)toa giza la shetani(Roho),
(njoo)Njoo roho kiongozi wetu twongoze katika njia safi(utukinge) utukinge na shetani
KIITIKIO:
4.Manabii wa uwongo (jamani) sasa waizunguka Dunia
Wanapotosha ukweli(jamani) wahubiri nguvu za shetani
(wao)Wajifanya ni mitume maandiko kupotosha wanatuangamiza
(njoo)njoo Roho Mtakatifu(njoo) twangazie mwanga wako(njoo)
(tupe) tupe uwezo wa kuelewayaliyo mabaya na mazuri (tuepushe)manabii wa uwongo
KIITIKIO:
5. Ujambazi uporaji(jamani) vimezidi katika jamii
Utapeli umezidi(jamani) ni nani aliye mwaminifu
(Kweli) ndugu wanaumizana upendo wa kweli hakuna mbona twaumizana
(njoo) njoo roho mtakatifu (njoo)kaa kwetu twakuomba(njoo)
(twaomba)utukinge na maovu yote Shetani ametuelemea
(twatamani) tuishi katika kweli
KIITIKIO: